**HALMASHAURI YA WILAYA YA KYERWA**

**MH MWENYEKITI,**

**Yah: TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA HALMASHAURI KIPINDI WAH MADIWANI WALIPOMALIZA MUDA WAO WA MADARAKA KWA KIPINDI CHA 2015 HADI 2020.**

## 1.0 UTANGULIZI

Mh mwenyekiti,

GN No. 430A/2020 ya tarehe 9 Juni 2020 ilitangaza rasmi kuvunjwa kwa mabaraza ya madiwani baada ya mabaraza hayo kufanya kazi kwa miaka 5 tangu mwaka 2015 hadi 2020

GN hiyo inataka shughuli zote zilizokuwa zinafanywa na Baraza la Halmashauri kufanywa na Kamati ya Menejiment na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya kuwa Mwenyekiti wa kamati ya uendeshaji ya Halmashauri ya Wilaya. Kwa kipindi chote cha miezi 5 ambacho madiwani hawakuwepo madarakani Timu ya Menejiment ya Halmashauri imeendelea kutekeleza majukumu mbalimbali kwa kuzingatia maelezo taratibu, miongozo kanuni na sheria. Hapa chini ni taarifa juu ya utekelezaji wa shughuri mbalimbali za Halmashauri

Kwa kipindi cha kuanzia Juni hadi Oktoba 2020 Halmashauri imeendelea kutekeleza bajeti mpya ya mwaka wa fedha 2020/2021 iliyokuwa imeidhinishiwa Tsh. 31,828,115,656.00 Shughuri zilizofanyika ni pamoja na utekelezaji wa miradi, Utekelezaji wa maagizo mbalimbali ya Serikali, Shughuri za uendeshaji na kufanya vikao mbalimbali vya kisheria ili kuamua maamuzi mbalimbali ya maendeleo kwa Halmashauri

## 22.0 TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

Halmashauri inaendelea kuhakikisha inatoa huduma bora kwa wananchi. Kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Halmashauri ya Wilaya Iliidhinishiwa kutumia kiasi cha Tshs.**31,828,115,656.00** kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbalimbali ikiwemo Mishahara, matumizi ya kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo jumla ya Tshs **7,876,715,496.00** ni fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya Maendeleo. Kiasi cha Tshs **1,114,454,387.73** kimetolewa na kiasi cha Tshs. **1,005,911,970.75** kutumika kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kama ifuatavyo:-

| SM | Jina la Mradi | Chanzo cha Fedha | Fedha Tumika |
|---|---|---|---|
| 1. | Mpango wa Elimu bila Malipo Elimu Msingi | Serikali kuu | 276,308,000.00 |
| 2. | Mpango wa Elimu bila Malipo Elimu Sekondari | Serikali kuu | 150,733,000.00 |
| 3. | Mikopo kwa vikundi 3 vya akina mama, 2 vya vijana na 1 Watu wenye ulemavu | Mapato ya ndani | 27,000,000.00 |
| 4. | Ujenzi wa choo matundu 4 na Mfumo wa maji Nkwenda Sokoni | Mapato ya ndani | 8,499,500.00 |
| 5. | Ujenzi wa choo matundu 4 katika mnada wa Katera | Mapato ya ndani | 4,758,700.00 |
| 6. | Ujenzi wa kizuizi cha Nkwenda | Mapato ya ndani | 1,004,000.00 |
| 7. | Huduma ya tiba na matunzo kwa wagonjwa wanaoishi na maambukizi ya VVU | MDH | 88,938,895.75 |
| 8. | Kuziwezesha kaya masikini mahitaji muhimu ili waweze kujikwamua kimaisha | TASAF | 448,669,875.00 |

| | | |
|---|---|---|
| | **JUMLA KUU (A)** | **1,005,911,970.75** |

Na jumla ya fedha Tshs. **817,042,548.77** ni fedha zilizovuka mwaka (Bakaa 2019/2020) na zimetumika kutekeleza miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2020/20221kama ifuatavyo:-

| SM | Jina la Mradi | Chanzo cha Fedha | Fedha Tumika |
|---|---|---|---|
| 1. | Ujenzi wa vyoo matundu 7 kwa Zahanati zifuatazo:- Songambere, Rwabwere, Nkwenda, Rukuraijo, Kakanja, Kagenyi, Kyerwa, Kaisho, Kibingo na Murongo | SRWSS-Afya/Mazingira | 272,000,000.00 |
| 2. | Ujenzi wa matundu ya vyoo 7 na vyumba 02 vya madarasa S.S Isingiro, vyumba 02 vya madarasa S.S Nyabishenge na Bwalo S.S Mabira | EP4R | 187,700,000.00 |
| 3. | Ujenzi wa vyumba 14 vya madarasa katika shule za Msingi za:- Kyerete 2, Chanyangabwa 2, Isingiro 2, Kakanja 2, Juhudi 2, Kimuli 2 na Mukunyu 2 | EP4R | 303,489,000.00 |
| 4. | Ukamilishaji wa matundu ya vyoo katika shule za msingi 5 za:- Songambere, Kaisho, Kagenyi, Kaaro na Isingiro | SRWSS-E/Msingi | 53,853,548.77 |
| | **JUMLA KUU (B)** | | **817,042,548.77** |
| | **JUMLA KUU (A+B)** | | **1,702,082,319.52** |

**Jedwali:- Fedha za Miradi za Bakaa, Makisio,Pokelewa na Matumizi 2020-2021**

| Na | Mradi/Chanzo Cha Fedha | Makisio 2020-2021 (Tshs) | Fedha Tolewa (Tshs) | Fedha Matumizi Mpaka Novemba(Tshs) | Fedha Baki (Tshs) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Mfuko wa Jimbo | 65,057,000 | 0 | 0 | 0 |
| 2. | Ruzuku toka Serikali Kuu | 2,192,517,172 | 0 | 0 | 0 |
| 3. | Elimu bila Malipo Elimu Msingi | 828,924,000 | 276,308,000 | 276,308,000 | 0 |
| 4. | Elimu bila Malipo Elimu Sekondari | 452,200,000 | 150,733,000 | 150,733,000 | 0 |
| 5. | HSBF | 721,022,784 | 0 | 0 | 0 |
| 6. | Global Fund | 7,525,000 | 7,401,159.34 | 0 | 7,401,159.34 |
| 7. | SRWSS | 509,800,000 | 0 | 0 | 0 |
| 8. | MDH | 593,674,540 | 105,088,419 | 88,938,895.75 | 16,149,523.25 |
| 9. | Jambo BUKOBA | 4,000,000 | 0 | 0 | 0 |
| 10. | LANES | 122,451,000 | 0 | 0 | 0 |
| 11. | Fedha za TASAF | 1,586,864,000 | 448,669,875.00 | 448,669,875.00 | 0 |
| 12. | Fedha Miradi ya Maendeleo - Mapato ya Ndani | 792,680,000 | 126,253,934.39 | 41,262,200.00 | 99,253,934.39 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | **Jumla** | **7,876,715,496** | **1,114,454,387.73** | **1,005,911,970.75** | **122,804,616.98** |

**Miradi kwa fedha za Bakaa**

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | EP4R | 491,189,000.00 | 491,189,000.00 | 491,189,000.00 | 0 |
| 2. | SRWSS-E/Msingi | 53,853,548.77 | 53,853,548.77 | 53,853,548.77 | 0 |
| 3. | SRWSS- Afya Mazingira | 272,000,000.00 | 272,000,000.00 | 272,000,000.00 | 0 |
| 4. | MAPATO YA NDANI | 3,792,989.38 | 3,792,989.38 | 0 | 3,792,989.38 |
| | **Jumla** | **820,835,538.15** | **820,835,538.15** | **817,042,548.77** | **3,792,989.38** |

## 3.0 VIKAO VYA KISHERIA

Vimefanyika vikao vitano (5) vya Timu ya Menejimenti (CMT) na kujadili masuala ya fedha kuanzia Juni hadi Oktoba 2020 na kikao kimoja (1) cha robo ya kwanza cha tarehe 20/10/2020 kujadili mambo ya kamati zote za kudumu ambazo ni kamati ya fedha, uongozi na mipango, kamati elimu na afya na kamati ya ujenzi, uchumi na mazingira. Maazimio na utekelezaji wake ni kama ifuatavyo:-

**Kikao cha Timu ya Menejimenti (CMT) cha tarehe 30/07/2020**

**Azimio**: Ifanyike sense ya bodaboda kwenye vituo vyao vyote ili waweze kulipia leseni na usafirishaji.

**Utekelezaji**: Zoezi la kuwabainisha limeishaanza kwenye kata 8 ambazo ni kikukuru 22, Rukulaijo 36, Songambele 31, Murongo 22, Kyerwa 30, rwabwere 23, Kibingo 21 na Kakanja 24.

**Kikao cha Timu ya Menejimenti (CMT) cha tarehe 12/08/2020**

**Azimio**, Ifanyike tathmini ya uzalishaji taka na kuweka viwango vya malipo kwa kufuata uwezo wa uzalishaji taka.

Utekelezaji: Tathimini imefanyika:-

1. Nkwenda uzalishaji taka ni tani 33.8 kwa mwezi kiwango cha mchango ni shilingi 1000 hadi 10,000 kwa mwezi kulingana na uzalishaji wa taka kwa mwezi.
2. Mabira uzalishaji taka ni tani 16 kwa mwezi mchango shilingi 1000 hadi 2000 kulingana na uzalishaji wa kiwango cha taka kila mwezi.
3. Isingiro uzalishaji wa taka tani 18 kwa mwezi, kiwango cha michango ni 1000 hadi 2000 kulingana nan a kiwango cha uzalishaji taka kwa mwezi.

**Azimio**, Lifuatiliwe deni la ushuru wa kahawa linalodaiwa KDCU na kupata taarifa kikao kinachofuata.

Utekelezaji: Utekelezaji umefanyika mnamo tarehe 26/08/2020 KDCU walipelekewa hati ya madai (invoice) kwa ajili ya ushuru wa kahawa waliokusanya ambazo ni kg. 24,539,377 yenye thamani ya Tsh. 883,417,572 mpaka sasa zimelipwa Tsh. 300,000,000 tu

**Kikao cha Timu ya Menejimenti (CMT) cha tarehe 11/09/2020**

**Azimio,** Ufuatiliwe ushuru wa madini ili kuweza kuongeza mapato ya Halmashauri.

**Utekelezaji**: Ufuatiliaji umefanyika na tayari ushuru umeishaanza kukusanywa kwa kipindi cha Julai hadi Oktoba 2020 zimekusanywa Tsh. 302,000

**Azimio,** Yafuatiliwe mapato ya tozo ya kukodisha nyumba kwenye miji midogo ya Rubwera, Isingiro na Nkwenda

**Utekelezaji**: Utekelezaji utafanyika baada ya kutungwa na kupitishwa sheria ya kutoza kodi ya upangishaji wa nyumba.

**Kikao cha Timu ya Menejimenti (CMT) cha tarehe 20/10/2020**

**Azimio:** iwasilishwe taarifa ya ukusanyaji wa PoS zote zilizogawiwa kwa wakusanyaji wa mapato kwa maeneo mbalimbali katika Halmashauri ya Wilaya.

**Utekelezaji:** Utekelezaji umefanyika jumla ya PoS 51 zinatumika kukusanyia mapato na zimekusanywa Tsh. 20,551,570 kwa mwezi Oktoba 2020.

**Kikao cha Timu ya Menejimenti (CMT) cha tarehe 19/11/2020**

**Azimio,** Litengenezwe gari la Mkuu wa Wilaya ya Kyerwa lililopata ajali kulingana na ombi aliloleta tarehe 27/10/2020

**Utekelezaji:** Matengenezo ya gari namba STK 2895 umeanza kwa awamu ambapo awamu ya kwanza shilingi milioni 7 kati ya shilingi milioni 14 zinazotakiwa.

**Azimio:** Waitwe watendaji waliopewa PoS na kupatiwa elimu juu ya utumiaji wa PoS kwa usahihi ili kuepuka makosa yasiyo ya lazima**.**

**Utekelezaji**: Watendaji wa makusanyo kwa kutumia PoS wameitwa tarehe 24/11/2020 kupewa elimu ya matumizi sahihi ya PoS.

Mihtasari yote ipo kwa kumbukumbu za Halmashauri.

## 4.0 **ZIARA ZA VIONGOZI WA KITAIFA**

Mnao tarehe 30/09/2020 Wilaya ya Kyerwa ilitembelewa na Waziri Mkuu Mh Kasimu Majaliwa kuangalia masuala ya kisiasa na shughuli za Serikali zinazotekelezwa Wilaya ya Kyerwa. Pia mnamo tarehe 12/09/2020 Wilaya ya Kyerwa ilitembelewa na Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi Mh Dr Bashiru Ally kuangalia utekelezaji wa shughuli za Serikali pamoja na chama.

## 5.0. **MASUALA MENGINE**

### A) **Janga la moto shule ya msingi ya mfumo wa kiingereza Byamungu**

Shule ya msingi ya mfumo wa Kiingereza Byamungu ni mojawapo ya Shule binafsi zilizopo Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa. Shule ilianza mwaka 2017 kwa namba ya usajili **EM. 17377** kama shule ya awali na Msingi ya kutwa. Hadi kufika darasa la sita (VI) ikiwa na jumla ya wanafunzi **122,** yaani **Wav. 79** na **Was. 43.** Mnamo tarehe **14 Septemaba, 2020** Shule hiyo ililipuka moto na kusababisha vifo vya wanafunzi **10**

pamoja na majeruhi **6,** majeruhi hao walipelekwa hospitali ya Nyakahanga kati yao **5** walipewa rufaa ya kwenda hospitali ya Bugando kati ya hao waliopelekwa Bugando 1 alifariki, hadi kufikia tarehe 19/11/2020 wanafunzi wawili (2) waliruhusiwa na wengine 2 wanaendelea na matibabu. Gharama zote za mazishi na matibabu zimegharimiwa na Halmashauri.

**Hatua zilizochukuliwa baada ya tukio la kuungua moto shule msingi ya mfumo wa kiingereza Byamungu**

i) Mkuu wa Mkoa Kagera Mhe.Brigedia Jenerali Marco E. Gaguti alifunga shule kwa muda usiojulikana kuanzia tarehe ya tukio kwa lengo la kuondoa taharuki kwa wanafunzi.
ii) Wanafunzi waliobaki hai na salama walirejeshwa kwa wazazi wao
iii) Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa ilipokea tukio hilo kwa uzito wake, hivyo iliweka mikakati ya kufanya uchunguzi kwa shule zote za Msingi na Sekondari za kutwa na Bweni ili kujihakikishia miundombinu na mazingira ya uratibu wa zoezi la utoaji huduma za kijamii kwa wanafunzi.
iv) Seikali imefuta usajili wa shule hiyo tangu tarehe 24 Septemba 2020

**6.0 Taarifa ya uchaguzi mkuu 2020**

Mnamo tarehe 28/10/2020 ulifanyika uchanguzi mkuu kwa mujibu wa katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuchagua viongozi nafasi ya Madiwani, Wabunge na Rais. Wilaya ya Kyerwa uchaguzi ulienda vizuri na kupatikana viongozi ngazi ya Udiwani, Ubunge na Rais.

Tunampongeza Mhe. Dkt John Pombe Magufuli kuchaguliwa kwa kura nyingi sana kuwa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania

Tunampongeza Mhe. Innocent Seba Bilakwate kuchaguliwa kwa kura nyingi sana kuwa mbunge wa Jimbo la Kyerwa

Tunawapongeza madiwani wote walio chaguliwa kushika wadhifu huo wa kutumikia wananchi katika Kata zao ndani ya Halmashauri yetu

Katika uchaguzi uliofanyika Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa ilifanya uchaguzi kwenye kata 24 na walichaguliwa madiwani kwenye kata zote ikiwa Chama cha mapinduzi (CCM) kilishinda kata 21 na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kushinda kata 3. Kipindi cha uchaguzi kata 3 zilipita bila kupingwa ambazo ni kata ya Rukulaijo, Kamuli na Kakanja. Vilevile waliteuliwa madiwani viti maalum 8 Chama cha Mapinduzi (CCM) waliteuliwa madiwani viti maalum 7 na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kiti 1.

Mh mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

Shadrack Mhagama

**MKURUGENZI MTENDAJI**

**HALMASHAURI YA WILAYA**

**KYERWA**

;